




Swahili Colloquium  
Bayreuth



UNIVERSITÄT  
BAYREUTH

**KONGAMANO LA KISWAHILI LA ISHIRINI NA TANO**  
**&**  
**DUNIA YAO**

**Utopia/Dystopia: Imagining Society in Swahili Fiction**

**tarehe 17 hadi tarehe 20 mwezi wa tano mwaka wa 2012**

**Bayreuth, Iwalewa-House**

tarehe 18, mwezi wa nne,  
mwaka wa 2012

Wapendwa Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Asanteni sana kwa hamu yenu ya kuchangia katika Kongamano la Kiswahili la 25 na mada zenu za kuvutia. Leo tunawaletea barua ya pili ya mwaliko ikiambatanishwa na ratiba yetu ya Kongamano. Mwaka huu ratiba yetu ni tofauti kidogo na ratiba za miaka iliyopita. Kwa hivyo tunawaomba kusoma barua hii pamoja na ratiba kwa uangalifu.

Kwanza mwaka huu tutakuwa na warsha yenye anwani “Duna yao: Utopia/dystopia: Imagining Society in Swahili Fictional Writings” itakayokusanya mabingwa maalumu walioalikwa tarehe 17 (na itakayoendelea tarehe 18 na tarehe 19 pia), yaani kabla ya Kongamano lenyewe. Kongamano la Kiswahili litanza siku ya Ijumaa tarehe 18 baada ya chakula cha mchana na litaendelea siku ya Jumamosi na siku ya Jumapili. Mnakaribishwa kuja mapema zaidi na kusikiliza hotuba zitakazowasilishwa wakati wa warsha. Lakini mkija, tafadhali, mjiandikishe kwa haraka iwezekanavyo kwa njia ya baruapepe fupi kwa [k.greven@gmx.de](mailto:k.greven@gmx.de).

Madhmuni ya warsha inayofadhiliwa na shirika la Fritz Thyssen ni kumheshimu mwenzetu, Said A. M. Khamis, mtaalamu maalum wa fasihi ya Kiswahili, na Said Ahmed Mohamed, mwandishi na mshairi maarufu, ambaye atastaafu mwisho wa mwaka huu. Mada ya warsha itatuwezesha kuzungumzia michango ya Said Ahmed Mohamed kwenye uwanja wa fasihi na pia kuiangalia kwa upana zaidi na kuilinganisha na maandishi mengine ya kisasa pamoja na fasihi na utamaduni pendwa. Kipengele cha ubunifu wa wakati ujao kitaandaa jukwaa kwa Kongamano la Kiswahili litakalofanyika kwa mara ya 25 mwaka huu. Maadhimisho yake ni nafasi nzuri ya kuzingatia historia yake pamoja na miaka ijayo.

Zote mbili, Kongamano la Kiswahili na Warsha ya Dunia Yao, zitafanyika Iwalewa-House, (Münzgasse 9, tazama ramani chini). Warsha itaanza **Alhamisi tarehe 17 saa mbili na nusu**

**asubuhi.** Kongamano la Kiswahili litaanza siku ya Ijumaa tarehe 18 saa saba na nusu. Kutakuwa na malipo ya usajili ya € 10 kwa wasio wanafunzi na € 5 kwa wanafunzi. Muda wa kutoa makala utakuwa  **dakika 20** na  **dakika 10** za kujadili kila wasilisho la makala.

Mambo machache mengine kuhusu ratiba: Kabla warsha ya ‘Dunia Yao’ haijaanza, wageni na wenyeji wote wanaombwa wakutane pamoja siku ya **Jumatano** (siyo Alhamisi!)  **tarehe 16, saa moja jioni** katika mkahawa unaoitwa ‘**Delphi**’ uliopo katika Badstr. 14 (tazama ramani). Huko kutakuwa na chakula na vinywaji ambavyo watakaohudhuria watajinunulia wao wenyewe. **Alhamisi tarehe 17 saa mbili ya jioni** baada ya vitafunaji, waandishi Kyallo Wamitila, Ken Walibora na Said Ahmed Mohamed watasoma kutoka riwaya zao. Siku ya Ijumaa, msanii mjerumani-mkenya Ingrid Mwangi atachangia kwa njia ya sanaa za maonyesho. Siku ileile saa mbili usiku tunataka kuwaalika nyote kwa karamu itakayofanyika Iwalewa-House ili kusherekea maadhimisho ya Kongamano la Kiswahili. Itafunguliwa na Abbas Kubaff mshairi na mwanagenge (hiphop) maarufu kutoka Kenya. **Siku ya Jumamosi tarehe 19** John Kiyaya, mpiga picha kutoka Sumbawanga (ambaye amealikwa na Wafaransa wenzetu), atatuonyesha baadhi ya picha zake.

Ikiwa mna maswali kuhusu Kongamano la Kiswahili, msisite kumwandikia Sebastian Müller ([swahili@uni-bayreuth.de](mailto:swahili@uni-bayreuth.de)). Mkitaka kujua zaidi kuhusu warsha ya ‘Dunia Yao’, mwandikie Katharina Greven ([k.greven@gmx.de](mailto:k.greven@gmx.de)).

Karibuni sana Bayreuth.

Wenu wakweli,

Prof. Gabriele Sommer, Prof. Dr. Gudrun Mieke,  
Dr. Clarissa Vierke, Katharina Greven  
Afrikanistik I  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553556

Prof. Said A. M. Khamis, Sebastian  
Müller, Mirka Joellenbeck  
Literaturen in afrikanischen Sprachen  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553598

